

KUUSU : KU JULISHA MUUNGANO YETU KWENU NA KU OMBA MCHANGO NA MASHAURI

Posté par VIJANA - 18-08-2008 à 20:23

Jambo wa Eshimiwa ,

Muungano ya Vijana ya Kongo , ni muungano ya Vijana wote wa Kongo duniani pote na kwetu , ambao wanao amini kati maendeleo ya inchi yetu kwa ajili ya wema ya taifa letu . Sisi siyo wapasha habari tu ya maombolezo na manunguniko , bali sisi ni kikundi ya Vijana wenye kuelewa kama ni kazi yetu kuleta mchango yetu kwa ajili ya wema ya taifa letu na inchi yetu . Na kwa iyo sisi hatu amini mabadiliko kwa maneno tu , bali sisi tuna amini kama sote tuki ji unga pamoja na kila mutu , kila kikundi kuleta mchango wake ndio tuta ona mabadiliko kati maisha ya taifa letu na inchi yetu . Hatu lete mambo mapya , bali tuna taka ku tiya kwa matendo mawazo na kazi zenye wababu na mashujaa wa taifa na inchi yetu wali anza na yenye ndio ina weza okowa taifa na inchi yetu kwa kweli .

Tume anza kazi ya kupasha habari ya tumaini na kuku sanya Vijana wote kati inchi za ugeni na kwa sasa tuna amini kwamba ni wakati ku anza kazi kati Vijana kwetu .

Mawazo yetu ni , kutayarisha Vijana kati :

1. Kuteteya hali yote ya kukosewa eshima ya taifa na inchi yetu ; ku omba haki kwa ajili ya taifa letu , wa Mama na Dada zetu pia mali yetu ambao ime aribishwa na maadui wa taifa letu .
2. Kutuma habari kwamba udongo na inchi yetu siyo ya kuuza pia kushimamisha adui zetu , kati mawazo yaku aribu mila zetu na ku nyanganya udongo yawa babu wetu .
3. Kujenga taifa letu kati ukweli na uhaki kati ugawanyo ya mali ya inchi yetu . Sote , kila mukongomani bila ugauzi ; tuna pashwa kula na kufurahiya mema ya inchi yetu .
4. Kujifunza na kuti ya kwa matendo maarifa mapya kati : biashara , uongozi , kusaidiya taifa ...

Kwa mafupi iyo ndiyo mawazo ambayo inayo tuongoza na kwa ajili yenye tume amua kusimama na kujiunga pamoja ili kuleta mchango wetu mpaka tuna ona mabadiliko kati maisha ya watu wetu .

Basi tume amua kuwa pasha iyo habari sababu tuna amini kwamba hatu wezi anza kitu bila kuelewana na kuku baliana nanyi . Pia tuna itaji msaada yenu kama wazee na waongozi wetu ili kutu saidiya kupasha ii habari kwa vijana wenzetu na kuwa saidiya kuji tayarisha kati kuteteya haki ya taifa na inchi yetu . Tuna amini kwamba iyi kazi hakuna mwenye anaye weza mwenyewe, hata serekali na nyinyi Wazee bila Vijana . Basi tuna endeleya kuwa shukuru kwa kazi yote muna fanya ili kuleta msaada kwa Vijana na Taifa letu .

MUMOJA HATA WEZA KITU , BALI SOTE PAMOJA MAMBO ITA GEUKA KWA MEMA YA TAIFA LETU : IYO NDIYO AGANO LETU .

YOTE YA WEZEKANA KWA KILA A AMINIYE MAANA HAKUNA KITU KIGUMU KWA MWENYEZI MUNGU WETU .

Kwa jina la uongozi wa Muungano ,
Mumoja kati wengi ,
Mukenge Barhegine

Re:KUUSU : KU JULISHA MUUNGANO YETU KWENU NA KU OMBA MCHANGO NA MASHAURI

Posté par admin - 19-08-2008 à 23:11

Jambo wandugu

Nilitaka kuuliza siege yenu ni wapi na wanani ndio wanashirikiyana na nyinyi katika hiyi kazi yenu, naona ni kazi kubwa na ngumu ila nawaza but munatafuta kufikiya ako iko noble

Aksanti

Re:KUUSU : KU JULISHA MUUNGANO YETU KWENU NA KU OMBA MCHANGO NA MASHAURI

Posté par Genty - 20-08-2008 à 01:37

Nafikiri kama kweli muna agano ya kueshimika, lakini sijaelewa ginsi munatumika. Kwani vijana wa kikundi

wanakutanana na kutafakari kuhusu maendeleo? Ama tayari muna kazi ambazo zinaendeleya?
Aksanti

=====